# Kusali kwa kuomba kwa imani maombezi ya Mwenyeheri Petro Vigne

Rafael Casado, paroko wa Sasamón, Hispania, aliwasilisha tafakari ifuatayo kwa kikundi cha waabudu wanaokutana kila mwezi katika nyumba yetu,tafakari ifuatayo. Hizi ni dondoo ambazo zitaendelea…



«Tunapata ibada kuabudu ya usiku, katika nyumba hii, katika kanisa lake ... Na jengo hili lina uwepo maalum wa Mwenyeheri Petro Vigne. Ndani ya kanisa tuna sanamu yake. Kwenye kordo, kuna sentensi zake, vitabu vyake vidogo, vipeperushi. Pia tunapokea karatasi "*Neno la Petro Vigne kwa leo*", nk. Na, juu ya yote, Watawa ambao wapo kama mwendelezo. Ni vyema kwamba tunawafahamu, kwa sababu alikuwa "**mpenzi" mkubwa wa Ekaristi na wa kuabudu Ekaristi.** Kumfahamu kutatusaidia kuimarisha ibada yetu ya Kiekaristi...

**Sala** ambayo iko juu ya sura yake, mwanzoni, **inaelekezwa kwa Yesu Kristo**, na sio kwa Petro Vigne. Haisemi: "Padre Vigne sikiliza"... bali, ***Bwana Yesu Kristo, sikiliza.*** Tunapopokea picha tunaangalia kwanza picha, mchoro. Tunaamini kwamba sala itaelekezwa kwa mtakatifu katika picha. Lakini kiliturujia Kanisa huelekeza sala kwa Mungu kwa maombezi ya mtakatifu huyu...

… Katika sala hii, sentensi ya kwanza ni kwa ajili ya Yesu: ***"Bwana Yesu Kristo, wewe unayetutakasa kwa sakramenti yako ya mapendo, tunakusihi: sikiliza sala yetu ya unyenyekevu.*** »

*Bwana Yesu Kristo,*
*Wewe unayetutakasa na sakramenti yako ya mapendo, tunakusihi .*
*Usikie sala yetu ya unyenyekevu.*
*Kwa maombezi ya Mtumishi wako Mwenyeheri Petro Vigne, Padre mmisionari, mtume wa Ekaristi na Mwanzilishi wa Shirika la Masista wa Sakramenti Takatifu, tunakusihi utujalie neema tunazokuomba (…)*

Yesu ndiye kitovu cha imani na sisi ni wafuasi wake. Hili ndilo lililo msingi na kuu katika maisha ya Kikristo. Hata Watawa wa Sakramenti Takatifu si wanafunzi wa kwanza wa Padre Vigne, bali wa Yesu Kristo... **Kwa hakika sana, Padre Vigne husaidia kumfuata Yesu.** Na Watawa wa Sakramenti Takatifu, wakiwa wafuasi wa Yesu, pia ni wafuasi wa Mwenyeheri Peter Vigne. Lakini hakuna hata mmoja wetu katika Kanisa anayepaswa kupoteza mweleke wetu wa kimsingi: **Yesu**, ambaye **lazima awe rejeleo kuu la maisha yetu ...**

Mwanzoni mwa sala, inasemekana kwamba **Kristo hututakasa kwa njia ya Ekaristi**, anatufanya watakatifu kwa njia ya Ekaristi. Huu ni ukweli mkubwa. Hatufanyiki watakatifu kwa juhudi zetu, utakatifu si suala la ngumi, bali ni zawadi kutoka kwa Mungu, zawadi ya neema ya Mungu. Na tunamwomba Yesu asikie sala yetu, sala yetu ya unyenyekevu, kwa sababu tunapaswa kuomba kwa namna ya unyenyekevu.

Sala inaendelea: ***Kwa maombezi ya mtumishi wako, Mwenyeheri Petro Vigne...*** Watakatifu ni wapatanishi. Wako mbinguni na wanatuombea. Ni vyema kumwomba Mungu neema kwa njia ya upatanishi wa watakatifu. Wao ni **ishara ya upendo wa Mungu kwetu. »**

**BARUA PEPE** :Kupitia maisha ya Mwenyeheri Petro Vigne, ninamshukuru Mungu kwa kunisaidia kuishi maisha ya upendo na kuwa na moyo wa kujitoa kwa wahitaji bila kujibakiza. Asanteni sana masista wa sakramenti Takatifu kwa **neno hili ambalo linalisha imani yangu**. Caroline Petro Morogoro. TANZANIA


**WATAWA WA SAKRAMENTI TAKATIFU**
**NYUMBA MAMA : 113, AVENUE VICTOR HUGO 26000 VALENCE - UFARANSA**



**N° 03-04. 2025**
*Imetolewa: Shirika la Masista wa Sakramenti Takatifu*


# NENO Mwenyeheri PETRO VIGNE Leo



## Kutembea kwa uthabiti...katika unyofu!

*Katika miezi hii inayodhihirishwa na Kwaresima na sherehe za pasaka, Petro Vigne anatuachia kama programu inayoweza kututia changamoto na kutualika kufanya maamuzi fulani yanayofaa kwa ajili ya maisha yetu ya kikristo. Uthabiti, furaha kujitolea, utume. Kwaresima njema kuelekea Pasaka*

*« Utupe neema Ee Mungu wangu, tusiwe na mwelekeo wa kukuchukiza kamwe hata ikitubidi, kwa hilo, kupoteza sifa yetu, urafiki wa mtu, mali zetu zote, na hata maisha yetu ! Na kwa hivyo kitu hiki kilicholaaniwa hakitatutenganisha na wewe, ambaye ndani yake tutapata kila kitu ambacho tunaweza kupoteza katika maisha haya.*



*Croix "de Pierre Vigne" à Rochepaule*

***Nataka, Ee Mungu wangu**,*
*kuiga wale wanaokupendeza,*
*na kuwaongelesha,*
*kutembelea makanisa yako*
*ili kusikia sifa zako za kimungu,*
*na **kujiunganisha na wale wanaokuabud.***
*Nataka kuongea juu ya ukuu wako wa kupendeza.*

*Ah ! Jinsi ninavyoipenda nyumba yako ! Nipe neema ya kuweza kuchangia mapambo yake, matengenezo yake, kwani huruma yako inaonekana humo.*

*Niweke mbali na wale ambao wangenipoteza… niokoe na taabu zangu. Unijalie **nitembee kwa uthabiti katika unyofu wa fadhila** na hivyo maisha yangu yaongoze kila mtu kukuhimidi, na kukutukuza kupitia mpatanishi Yesu msulubiwa. »*

**H.N. 1-140-141**

Vigne ptre missionnaire

# Pamoja na Papa Fransisko

*Kwa muda wa siku kumi na tano zilizopita, tunamsindikiza papa wetu Fransisko na kumwombea akiwa katika hospitali ya Gemelli. Tupokee mwaliko wake utakaotusaidia kuishi Kwaresima.*

**NAMWALIKA KILA MKRISTO**, katika mahali na hali yoyote aliyonayo, kuupyaisha leo hii makutano yake binafsi na Yesu Kristo au, angalau kufanya uamuzi wa kujiruhusu kukutana naye, kumtafuta kila siku bila kuchoka.

Hakuna sababu ya mtu yeyote kufikiri kwamba mwaliko huu sii kwa ajili yake, kwa sababu « *hakuna mtu ambaye ametengwa na furaha ambayo Bwana anatuletea»* Yule anayejihatarisha, Bwana hamkatishi tamaa na **wakati mtu akifanya hatua ndogo kuelekea Yesu,** anagundua kwamba huyu tayari alikuwa akisubiri kuwasili kwake na miko wazi..

**Huu ndio wakati** wa kumwambia Yesu Kristo : *« Bwana nimejiacha kudanganywa, kwa njia elfu moja nimeukimbia upendo wako, lakini bado niko hapa kwa mara nyingine tena ili kufanya upya agano langu na wewe. Nakuhitaji. Unikomboe tena bwana, unipokee kwa mara nyingine tena katika mikono yako ya ukombozi ».*

**Hili linatusaidia sana kurudi kwake** wakati tunapojipoteza wenyewe!

Mungu hachoki kusamehe, ni sisi tunaochoka kuomba huruma yake…

**Tusikimbie ufufuko wa Yesu,** tusikate tamaa kamwe, hata iweje. Hakuna kinachoweza kufanya zaidi ya maisha yake ambayo yanatusukuma mbele!

Furaha ya Injili 3

# Kwaresima ya kuishi

Tarehe 5 Machi tunaingia kipindi cha Kwaresima. Kama mitume waliomfuata Kristo, tumeitwa kujiachia kusukumwa huku na huku. Kila mtu anaalikwa kupiga hatua moja zaidi kuelekea Kwake na pamoja Naye ambaye, kwa Upendo, alitoa maisha yake kwa ajili yetu.

Petro Vigne anaomba neema ambayo haijapoteza umuhimu wake : *« kwamba hii imelaaniwa watu watasema nini kamwe haitutenganishi na wewe »* ! **Je utaishi Kwaresima kwa uwazi au unapendelea tusijue lolote?**

Kila Ijumaa utaweza kuonesha kuwa ni Siku maalum: kwa mfano, hakuna nyama kwenye chaakula?



Ijumaa…ni siku ambayo itapendekezwa nyakati za sala mbele ya Msalaba au Njia ya Msalaba...
Je utashiriki ?
***"Nataka, Ee Mungu wangu, nijiunganishe na wale wanaokuabudu."***

Tunaishi, wewe na mimi, sote, katika jamii ngumu, yenye wasiwasi, iliyoharibiwa na vurugu, vita, ugaidi, katika ngazi ya kimataifa na pia karibu.

Kwaresima ni wakati wa kusahihisha kile ambacho labda kimepotosha au kupotoshwa katika maisha yangu; muda wa kuwa mwaminifu zaidi,- « imara »-, wa kuunganisha matendo yetu na imani yetu. Hizi siyo droo mbili zinazopingana au zinazofungana kila moja! **Ni lazima kuthubutu kuishi « NINAAMINI » yetu kwa uthabiti, *« na hivyo,-Mungu wangu- maisha yangu yaongoze kila mtu kukuhimidi na kukutukuza.»***

Sala, toba, ushuhuda **katika mahujaji wa matumaini»,** *siku* 40…na zitakuja siku takatifu, na ALELUYA ya Pasaka . *B.R.*

# Tusali kwa ajili ya Papa Fransisko



*…na tuupokee ujumbe huu :*

« …kumfahamu Yesu si sawa na kutokumfahamu,
kutembea naye si sawa na kupapas,
kuwa na uwezo wa kumsikiliza au kupuuza Neno lake havifanani…
kuwa na uwezo wa kumtaamuli, kumwabudu,
kutulia ndani yake, au kutoweza kufanya hivyo havifanani. Kujaribu kujenga ulimwengu kwa Injili yake si sawa na kujenga kwa sababu zake mwenyewe. Tunajua vizuri kwamba pamoja naye maisha yanakuwa kamili zaidi, na kwamba pamoja naye ni rahisi zaidi kupata maana katika kila kitu.

Fransisko – Furaha ya Injili 266

## KUSALI NA LITURUJIA



*Umetuambia, Bwana,*
*kumsikiliza Mwanao Mpendwa,*
*utufanye tupate katika Neno lako*
*chakula ambacho imani yetu inakihitaji...*
***Wewe ndiwe chanzo cha wema wote,***
*na rehema zote zatoka kwako …*
*tunafahamu makossa yetu,*
***kwa subira tuinue kwa upendo wako.***
*neema yako itupatie kuiga*
*kwa furaha upendo wa Kristo,*
*aliyetoa maisha yake kwa upendo kwa ajili yetu.*
*Kupitia adhimisho la Pasaka huisha tena*
*imani yetu na ongeza ndani yetu neema*
*yako. Amina*

# Neno la Mungu

Mwanangu,
ukija kumtumikia Bwana,
weka tayari moyo wako kwa kujaribiwa.
**Ujitengeneze moyo ustahimili,**
jizatiti kwa ujasiri,
wala usitaharuki, siku ya kuteswa.
Uambatane naye wala usijitenge tena,
ili mwisho wako ukuzwe.
Kila utakalopelekewa ulipokee kwa
kuchangamka moyo…,
Uyavumilie mabadiliko ya unyonge wako…
**Weka imani yako kwa Mungu**
naye atakusaidia,
**ukazinyoshe njia zako** na kulikaza
taraja lako kwake.
Yoshua Bin Sira 2 : 1-6



**Miezi miwili muhimu ya kusherehekea Imani yetu katika Kanisa**

<u>5 Machi</u>: **Jumatano ya Majivu. Mwanzo wa Kwaresima**. Safari ya siku 40 na inayotuongoza kuelekea Pasaka.

19 Machi :sikukuu ya **Mtakatifu Yosef** *«nendeni karibu naye na igeni maisha yake ya kawaida. »*

25 Machi :sikukuu ya **kupashwa Habari**…na Maria akawa *« Tabernakulo nzuri ya Mungu »*

**13 Aprili : Jumapili ya Matawi, ya Mateso.** *Hosana*

17-18-19 Aprili : **Siku Takatifu**: Ekaristi, Mateso-*Msalaba. Ukimya na kukesha.* (Njia ya Msalaba huko Boucieu)

**20 Aprili** : Sikukuu Kubwa ya PASAKA . **Furaha ya Ufufufko wa Yesu.**